# Mradi wa kunusuru vyanzo vya maji kupitia matumizi bora ya ardhi




Bodi ya maji bonde la wami/ruvu kupitia wizara ya maji na mfuko wa fedha kutoka shirika la kimataifa la maendeleo (UNDP) na mfuko wa mazingira wa dunia (GEF, inatekeleza mradi wa kunusuru vyanzo vya maji kupitia matumizi bora ya ardhi katika kidaka maji cha Ruvu (Kielelezo). Mradi huu wa miaka mitano (2016 – 2020) unatekelezwa katika kidakio cha Ruvu mkoani Morogoro na Zigi mkoani Tanga.

Baadhi ya kazi zilizowahi kufanyika katika kidaka maji cha Ruvu ni hizi zifuatazo,

- Kuanzishwa kwa Jumuiya (4) za watumia maji ambazo ni mgolole, mbezi, mvuha juu na mvuha chini.
- Kuundwa kwa Jukwaa na kamati za watumia maji wa kidakio kidogo cha ngerengere.
- Utoaji wa pikipiki nne (4) kwa jumuiya za Mfizigo, Ngrengere chini, Ngerengere Juu A, na Mgolole.
- Utoaji wa mashine ya kufyatulia matofali kwa ajili ya ujenz wa ofisi za jumuiya



- Utoaji wa mizinga ya nyuki 350 kwa makundi nane (8) ya wajasiriamali, jumuiya tano (5) na COWSO.

-  

Kuweka mipaka ya mita 60 kwenye mito Mfizigo, Mvuha na Ruvu. Uwekaji huu ni wakutumia concrete bicon kwa nafasi ya mita 100 kila nguzo.

